

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

Simu: +255262963470  
Barua Pepe: [ps@mit.go.tz](mailto:ps@mit.go.tz)  
Barua Pepe: [gcu@mit.go.tz](mailto:gcu@mit.go.tz)  
Tovuti: [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz)  
Nukushi: +255262963117



Mji wa Serikali,  
Mtumba,  
Mtaa wa Viwanda,  
S.L.P 2996,  
40478, Dodoma.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA CAMARTEC

07 Septemba, 2021, DODOMA.

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Prof. Kitila A. Mkumbo (Mb.), kwa Mamlaka aliyo nayo kwa mujibu wa Sheria ya CAMARTEC Na. 19 ya mwaka 1981 na Marekebisho yake ya mwaka 2019 ameteua Wajumbe nane (8) wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC). Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Valerian Cosmas Kanyengele Silayo aliteuliwa na Mamlaka husika tarehe 16 Juni 2021.

Wajumbe walioteuliwa na Waziri Mkumbo ni kama ifuatavyo:

1. Prof. Karoli N. Njau, *Mhandisi Mazingira*, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST);
2. Bw. Jovinary W. Rwemigira, Meneja wa Mipango na Fedha, Taasisi ya Uhasibu Arusha;
3. Bi. Nina H. Nchimbi, Meneja wa Mkoa wa Arusha, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO);
4. Dkt. Joseph C. Ndunguru, Mkurugenzi wa Kituo cha Arusha (Selian), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI);
5. Dkt. Musa N. Chacha, Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha;
6. Dkt. *Mhandisi* Yuda L. Benjamini, Mkurugenzi Msaidizi Utafiti na Ubunifu, Wizara ya Viwanda na Biashara;
7. *Mhandisi* Bi. Motta R. Kyando, Meneja wa Mkoa wa Kilimanjaro, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS); na
8. Bi. Ziana T. Mlawa, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Wizara ya Nishati.

Uteuzi wa Wajumbe hao utadumu kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia tarehe 06 Septemba, 2021.

Imetolewa na:

A handwritten signature in purple ink, appearing to read 'Suzan C. Mshakangoto'.

Suzan C. Mshakangoto  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Wizara ya Viwanda na Biashara